

Aprili 7, 2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Tumerudi shuleni! Tunajua watoto wenu wamefurahia kurudi ili kuwasiliana na walimu wao na wanafunzi wenzao kama tulivyorejelea mwaka wa shule wa 2019-20 kwa kutumia Mafunzo Yasiyo ya Kiasili (NTI). Walimu wanajishughulisha na kuwasiliana na wanafunzi na kila mmojo wao kuelewa teknolojia mpya na kutayarisha masomo ya wiki zijazo za kusoma nyumbani. Lakini, muhimu zaidi, wanaelewa, ni wepesi na wako tayari kusaidia mtoto wako kwa njia yoyote wanayoweza kufanya uzoefu wa wa kujifunza NTI kuwa mzuri iwezekanavyo. Na hilo maanani, hapa kuna sasisho chache kutoka JCPS:

- Familia ambazo ziliitisha Chromebooks kwa mafanikio watazipokea mwishoni mwa wiki au mwanzoni mwa wiki ijayo. Tumetuma karibu nusu ya takriban kompyuta 20,000 ambazo tumedhibitisha za kusambazwa kwa familia katika mipango ya Chakula cha Mchana cha Bure au Kilichopungzwa au Elimu ya Kipekee ya Mtoto (ECE). Tutawasiliana na familia za ECE kuhakikisha wako na Chromebook au kompyuta nyingine nyumbani ya kushiriki vikao vya matibabu ya mtu binafsi mtandaoni na pia kazi ya shule. Tunaendelea kuunda mpango wa kusambaza vidude vya mtandao kwa familia wanaohitaji.
- Ikiwa Chromebook yako haijwasili au hauma kompyuta nyumbani, hakuna haja ya wasiwasi. Mtoto wato ataendelea kushiriki katika NTI kupitia nakala zilizochapishwa za Choice Boards ambazo zina mazoezi maalum ya daraja za kufanywa na wanafunzi. Zinaweza kuchukuliwa katika zaidi ya Viwanda vyetu 60 vya [Chakula cha Dharura](#). Choice Boards pia zinaweza kufikiwa kwa simu ya rununu katika: <https://apps.jefferson.kyschools.us/orchard/JCPS-Choice-Board-Portal>. Walimu watakuwa wanawafikia wanafunzi wetu hii wiki na maagizo zaidi ya wanafunzi.
- Kuanzia wiki ijayo Jumatano, Aprili 15, pakiti zilizochapishwa za mazoezi ya kielimu yatapatikana katika viwanda vya chakula pamoja na Choice Boards.
- Tembelea [wavuti](#) hii ikiwa unahitaji msaada wa kiufundi au ikiwa una maswali mengine ya kiteknolojia.
- Unaweza kutafuta shule ya mtoto wako, mwalimu na kazi ya shule kwa kubonyeza [hapa](#). Hii ni wavuti muhimu sana kwako na kwa mtoto wako kupata. Ukurasa kuu wa JCPS NTI uko hapa: <https://sites.google.com/jefferson.kyschools.us/jcps-nti/home>
- Wengi wa watoto wenu wamewasiliana na mwalimu/walimu wao. Ikiwa wanafunzi wana maswali kuhusu kazi ya shule ya NTI na wasipowasiliana kwa njia yoyote na mwalimu hadi mwisho wa wiki hii, tafadhali wasiliana na mwalimu. Ikiwa huna bahati yoyote, wacha ujumbe wa simu kwa shule ya mtoto wako na mtu atakupigia simu.
- Walimu wetu wanafanya kazi kwa bidii, kuzoea na kujifunza mambo mapya kwani wamejitayarisha kwa siku za mwanzo za mafunzo ya nyumbani kwa wanafunzi walio nyumbani. Janine Hogan ni mwalimu wa daraja la 1 katika Maupin Elementary: <https://www.youtube.com/watch?v=I5bSlIu4RSc&t=5s>.
- Asante kwa kufanya #WeAreJCPSatHome mada inayoongoza leo kwenye mitandao za kijamii! Ikiwa hutufuati kwenye mitandao ya kijamii, hakikisha kufuata mambo yote ya JCPS kwenye Facebook (Shule za Umma za Kauti ya Jefferson), Twitter (@JCPSKY), na Instagram (@JCPSKY).

Tunatumai barua pepe hizi za mara kwa mara zinajibu maswali yenu mingi, kuwapa habari mpya za kinachoendelea JCPS na jinsi itakavyoadhiri mtoto wako katika wakati huu wa kipekee katika historia. Tafadhali kuwe mwenye busara, kaa na afya na himiza mtoto wako kujitahidi wakati huu wamerudi shuleni (kutoka nyumbani).